SAUTI YA TSC

TOLEO NA.19 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) SEPTEMBA 2022

WAZIRI MKUU AZINDUA VITABU VYA KIMKAKATI KUBORESHA ELIMUMSINGI, SEKONDARI

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) (kulia) akizindua vitabu vitatu vya kimkakati vya kutoa miongozo na mikakati ya kuboresha Elimu Msingi na Sekondari pamoja na kuimarisha uongozi katika Ngazi za Shule, Kata, Halmashauri na Mikoa wakati akifungua mashindano ya michezo katika Shule za Msingi (UMITASHUMNTA) pamoja mashindano ya michezo katika shule za Sekondari (UMISSETA) tarehe 04 Agosti, 2022 Mkoani Tabora. Pembeni yake ni Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. David Silinde.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

VITABU VYA MIONGOZO NA MIKAKATI YA KUBORESHA ELIMU VITUMIKE KULETA MAGEUZI YA ELIMU NCHINI

Hivi karibuni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) alizindua vitabu vitatu vya kimkakati vya kutoa miongozo na mikakati ya kuboresha Elimumsingi na Sekondari pamoja na kuimarisha uongozi katika Ngazi za Shule, Kata, Halmashauri pamoja na Mikoa.

Kitabu cha kwanza kinahusu Mwongozo wa Uteuzi wa Viongozi wa elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa ambapo kimeainisha taratibu zinazopaswa kuzingatiwa katika kuteua viongozi wa elimu ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa.

Kitabu cha pili kinahusu Changamoto katika Uboreshaji wa Elimu Msingi na Sekondari na kile kinachotakiwa kufanyika ambapo kimebainisha changamoto kuu za utekelezaji wa maboresho ya ufundishaji na ujifunzaji pamoja na hatua zinavopaswa kuchukuliwa na viongozi wa elimu kutoka ngazi zote kuanzia ngazi ya shule hadi Taifa.

Kitabu cha tatu kinahusu kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi ya elimu msingi ambapo kitabu hicho kimelenga kuwawezesha wataalam na walimu kubaini changamoto za kina za ufundishaji na ujifunzaji zilizopo, athari za changamoto hizo, fursa zilizopo pamoja na kutumia mikakati ya utatuzi wa changamoto hizo.

Lengo la kuandaliwa kwa vitabu hivi ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata ujuzi unaotakiwa ili kuendelea kuinua kiwango cha elimu nchini. Ni wazi kuwa uandaaji wa mikakati hii ni jambo moja na utekelezaji wake ni jambo jingine. Wito wetu kwa mamlaka zote zinazohusika na usimamizi wa elimu ni kuhakikisha kuwa mikakati na miongozo hiyo inatekelezwa kikamilifu kuanzia ngazi ya shule ili tuendelee kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya elimu.

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Paulina Nkwama

Wajumbe
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya
Zachary A. Dida

Mhariri Mkuu
Gerard Chami

Mhariri
Adili Mhina

Msanifu Kurasa
Lucas Gordon

KATUNI



Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***
Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

WAZIRI MKUU AZINDUA VITABU VYA KIMKAKATI KUBORESHA ELIMUMSINGI, SEKONDARI

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dkt. Charles Msonde akitoa maagizo mbalimbali kwa Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya (hawapo pichani) wakati wa kikao chake na maafisa elimu hao kilichofanyika Agosti 10, 2022 mjini Tabora.

Na Mwandishi wetu – Tabora.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) amezindua vitabu vitatu vya kimkakati vya kutoa miongozo na mikakati ya kuboresha Elimumsingi na Sekondari nchini pamoja na kuimarisha uongozi katika Ngazi za Shule, Kata, Halmashauri pamoja na Mikoa.

Vitabu hivyo vimezinduliwa rasmi katika Ufunguzi wa mashindano ya michezo ya Shule za Msingi (UMITASHUMNTA) pamoja mashindano ya michezo ya shule za Sekondari (UMISSETA) tarehe 04 Agosti, 2022 Mkoani Tabora.

Akisoma taarifa yake Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. David Silinde amesema kuwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliunda kikosi kazi kilichobainisha changamoto zote za uendeshaji wa Elimumsingi na Sekondari pamoja na kutoa mwongozo wa nini kifanyike ili kuboresha elimu nchini.

"Kupitia uchambuzi huo uliofanywa na kikosi kazi Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeandaa vitabu vitatu vitakavyotoa miongozo na mikakati ya kuboresha Elimu Msingi na Sekondari nchini pamoja na kuimarisha uongozi katika ngazi za Shule, Kata, Halmashauri na Mikoa nchini" alisema Mhe. Silinde

Akivitaja vitabu hivyo Mhe. Silinde alisema kitabu cha kwanza kinaitwa Mwongozo wa Uteuzi wa Viongozi wa elimu katika

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dkt. Charles Msonde (katikati) akiwa pamoja na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kushoto) na viongozi wengine wa Elimu kutoka OR – TAMISEMI wakati wa kikao kilichowakutanisha Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya (hawapo pichani) Agosti 10, 2022 mjini Tabora.

WAZIRI MKUU AZINDUA VITABU VYA KIMKAKATI KUBORESHA ELIMU MSINGI, SEKONDARI

Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa huku akibainisha kuwa kitabu hicho kimeainisha taratibu zinazopaswa kuzingatiwa katika kuteua viongozi wa elimu ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa ili kwa kupitia vigezo vilivyoainishwa wapatikane viongozi wenye weledi katika kusimamia masuala ya elimu.

"Kitabu cha pili kinaitwa Changamoto katika Uboreshaji wa Elimu Msingi na Sekondari na Nini Kifanyike. Kitabu hiki kimebainisha changamoto kuu za utekelezaji wa ufundishaji na ujifunzaji pamoja na hatua zinazopaswa kuchukuliwa na viongozi wa elimu ngazi zote kuanzia ngazi ya shule hadi Taifa" alisema Mhe. Silinde

Aliendelea kufafanua kuwa kitabu cha tatu kinahusu kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi ya elimumsingi ambapo amelisema kuwa kitabu hicho kimelenga kuwawezesha wataalam na walimu kubaini changamoto za kina za ufundishaji na ujifunzaji zilizopo, athari za changamoto hizo, fursa zilizopo pamoja na kutumia mikakati ya utatuzi wa changamoto hizo.

"Vitabu hivi vya kimkakati vimelenga kila msimamizi wa elimu Msingi na Sekondari kuhakikisha anazidisha ubunifu na weledi katika ufundishaji wenye kuleta tija inayotarajiwa kwa mwanafunzi mmoja mmoja kwa kutumia mbinu mbalimbali zikiwemo michezo na Sanaa za Maonesho" alisisitiza Mhe. Silinde

Katika kuhakikisha vitabu hivyo vinawafikia walengwa, Agosti 9, 2022 Naibu Katibu Mkuu (Elimu) Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Dkt. Charles Msonde alikutana na Maafisa Elimu Msingi na Sekondari na kuwataka kuhakikisha wanawashirikisha wadau wote wa elimu katika utekelezaji wa miongozo iliyopo katika vitabu hivyo ili kuleta uelewa wa pamoja na kuimarisha umahiri wa mwanafunzi mmoja mmoja.

"Hakikisheni mnawashirikisha vizuri wadau wote wa elimu waliopo katika kila ngazi kuanzia ngazi ya Kata, Halmashauri Pamoja na Mkoa mikakati iliyotolewa na kuwapa mbinu bora ya kutekeleza mikakati hiyo ili kuleta mageuzi katika elimu lakini pia kuimarisha umahiri wa mwanafunzi mmoja mmoja" Dkt.

Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama akiongea na Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya (hawapo pichani) katika kikao kilichofanyaika mjini Tabora Agosti 10, 2022.

WAZIRI MKUU AZINDUA VITABU VYA KIMKAKATI KUBORESHA ELIMU MSINGI, SEKONDARI

Maafisa Elimu wakimsikiliza kwa makini Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama katika kikao kilichofanyaika mjini Tabora Agosti 10, 2022.

Msonde

Agizo hilo alilitoa katika Kikao kazi kilichofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Ualimu Mkoani Tabora ambacho kililenga kuleta majadiliano ya pamoja ya namna bora ya kutekeleza miongozo iliyopo katika vitabu hivyo vilivyozinduliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) Agosti, 4, 2022.

Aidha, aliwataka Maafisa hao kuhakikisha wanasimamia uteuzi wa viongozi wa Elimu kwa kufuata miongozo wa uteuzi wa viongozi wa elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa ulioweka bayana sifa za uteuzi wa viongozi ili kuepuka viongozi wenye utendaji hafifu.

Vilevile amewataka viongozi wote wa elimu nchini kufanya ufatiliaji wa kina wa namna gani mwanafunzi anapata umahiri katika masomo na kuandaa mkakati wa kuhakikisha kila mwanafunzi anapata ujuzi uliokusudiwa na Serikali.

Sambamba na maagizo hayo, alielekeza kuwa kila mwalimu wa shule ya Msingi na Sekondari ahakikishe anajiwekea malengo na mpango kazi na kuhakikisha kila mwanafunzi anapata umahiri katika masomo yake akisitiza kuwa malengo ya mwalimu yana nafasi kubwa katika kuleta mageuzi kwa kila mwanafunzi na shule kwa ujumla.

Mkutano huo ulihudhuriwa na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama ambapo aliwasisitiza Maafisa Elimu kushughulikia masuala ya walimu kwa wakati ili waendelee kuwa na moyo wa kufanya kazi kwa weledi, uzalendo na ubunifu zaidi kwa lengo la kuwafanya wanafunzi kupata ujuzi unaohitajika.

Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya wakiwa katika hali ya utulivu wakati wa kikao chao na Naibu Katibu Mkuu wa OR – TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Dkt. Charles Msonde (hayupo pichani).

KATIBU TSC AFANYA ZIARA KWENYE OFISI ZA TSC CHUNYA, MBARALI, URAMBO, KALIUA, SIKONGE

Na Mwandishi wetu.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama amefanya ziara katika Wilaya za Chunya, Mbarali, Kaliua na Urambo kwa nyakati tofauti kwa lengo la kufanya ufuatiliaji wa namna ofisi hizo zinavyofanya kazi katika kutoa huduma kwa walimu kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016.

Katika ziara hizo, Nkwama amesisitiza watumishi wa Tume kuhakikisha wanafanya kazi kwa weledi na ubunifu katika kutoa huduma kwa walimu ili kufanya walimu wabaki kwenye vituo vyao vya kazi badala ya kuhangaika kwenye ofisi mbalimbali kutafuta huduma.

Aliongeza kuwa kwa sasa TSC iko mbioni kukamilisha mfumo wa kielektroniki (TSCMIS) wa kuwahudumia walimu ambao utawafanya kuwasilisha changamoto zao kwa njia ya mtandao bila kulazimika kufika kwenye ofisi za Tume.

"Tupo kwenye hatua za mwisho za kuanza kutumia mfumo wetu wa TSCMIS katika kutoa huduma kwa walimu. Kupitia mfumo huo, walimu wataweza kuwasilisha masuala yao kupitia simu zao za mkononi na sisi tukazifanyia kazi kwa wakati. Kwa hiyo walimu hawatakuwa na haja tena ya kuondoka kwenye vituo vyao vya kazi, badala yake huduma hiyo itawafuata mahali walipo" alisema Mwl. Nkwama.

Nkwama aliendelea kueleza kuwa Menejimenti ya TSC inaendelea kuangalia namna ofisi za Wilaya zitakavyoweza kuunganishwa na mfumo huo kwa kuwa kwa sasa ofisi nyingi hazijaunganishwa na mtandao wa intaneti.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama.

Katika ofisi alizotembelea, Mwl. Nkwama amebaini uwepo wa upungufu wa watumishi na vitendea kazi. Changamoto hizo zimeendelea kushughulikiwa ambapo Ofisi ya Rais TAMISEMI imeendelea kuiwezesha TSC watumishi kutoka kwenye MSM kutoa huduma kwa walimu, vitendea kazi pamoja na ujenzi wa mfumo wa TSCMIS ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa haraka zaidi..

Aidha, kuhusu changamoto ya uchakavu wa miundombinu, utatuzi wake unaendelea kushughulikiwa kwa kupatiwa Ofisi katika mojawapo ya Ofisi za Halmashauri/ wilaya husika.

Kuhusu upungufu na uchakavu wa vitendea kazi, Nkwama alieleza kuwa Tume hiyo imefanya jitihada kubwa za kununua Kompyuta na samani za ofisi kwa ajili ya ofisi zake za wilaya. Hata hivyo alifafanua kuwa zoezi hilo ni endelevu na ofisi zenye changamoto zitanunuliwa vitendea kazi kwa kadiri fedha zinavyopatikana.

Pamoja na hayo alieleza kuwa TSC ilinunua pikipiki 81 na kuzigawa kwenye baadhi ya ofisi za wilaya kwa ajili ya kurahisisha usafiri, na kusema kuwa imeonekana kuwa bado kuna uhitaji mkubwa wa vyombo hivyo vya usafiri katika Wilaya mbalimbali. Hivyo, katika bajeti ya mwaka huu (2022/2023) TSC imetenga shilingi 197,200,000 kwa ajili ya kununua pikipiki zingine na kuzisambaza katika ofisi zake.

TSC KYELA YAONGEZA UBUNIFU KUHUISHA TANGE YA WALIMU

Na Mwandishi wetu – Kyela.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama amepongeza watumishi wa TSC Wilaya ya Kyela iliyoko mkoani Mbeya kwa kuweka utaratibu wa kushirikisha walimu ili kupata taarifa sahihi kwa lengo la kuhuisha tange ya walimu hao kwa ufanisi.

Nkwama alitoa pongezi hizo hivi karibuni wakati wa ziara yake katika Ofisi ya TSC Wilaya ya Kyela iliyolenga kufanya ufuatiliaji wa namna ofisi hiyo inavyowajibika katika kutoa huduma kwa walimu wa shule za msingi na sekondari walioajiriwa na Serikali katika Wilaya hiyo.

Ubunifu huo uliomfurahisha Katibu wa TSC unahusisha Ofisi hiyo kuandaa fomu yenye taarifa za walimu zilizopo kwenye kanzi data ya ofisi hiyo kwa kila shule na kuwapatia walimu ili kila mmoja ahakiki taarifa zake na kufanya marekebisho pale anapoona taarifa yake haipo sawa jambo ambalo limefanya Wilaya hiyo kuwa na tange iliyohuishwa kwa usahihi.

Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (kulia) akizungumza na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kyela, Julius Mwambogela kuhusu utaratibu unaotumiwa na Ofisi ya Wilaya hiyo kupata taarifa kwa ajili ya kuhuisha Tange ya Walimu.

Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (kulia) akimwonesha Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kyela, Julius Mwambogela Kifungu cha 14 (3) cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya Mwaka 2015 kinachosisitiza kuwa na vikao vya mashauriano baina ya TSC na Mkurugenzi wa Halmashauri ili kuboresha utoaji wa huduma kwa walimu.

"Utaratibu mliouweka ni mzuri kwa kuwa unafanya kuwa na tange ya walimu inayoendana na uhalisia. Najua kuna walimu wamejiendeleza lakini wakati mwingine hawaleti taarifa zao, sasa utaratibu huu utasaidia pia kujua kama kuna walimu wana sifa za kubadilishiwa muundo wakasimiwe kwenye bajeti na kubadilishiwa kwa wakati stahiki," alisema Nkwama.

Nkwama alieleza kuwa ili kuondoa kero za walimu ni lazima watumishi wa TSC kuwa wabunifu, kufanya kazi kwa bidii na moyo wa kujituma huku akiwasisitiza watumishi wa ofisi

TSC KYELA YAONGEZA UBUNIFU KUHUISHA TANGE YA WALIMU

hiyo kushirikiana na watumishi wa wilaya za jirani ili nao waweze kutumia mbinu hiyo katika kuboresha taarifa za walimu pamoja na kupeana uzoefu wa namna ya kuwahudumia walimu kwa ubora zaidi.

"TSC bado tunahitaji kujengeana uwezo, hivyo kwa kuwa ninyi mmefanikiwa katika utaratibu wa kuboresha tange ya walimu, wasilianeni na wenzenu wa wilaya jirani na kuwashirikisha namna mnavyofanya ili nao wafanye vizuri katika kuhuisha tange za walimu pamoja na maeneo mengine tunayotoa huduma kwa walimu," alisisiza Nkwama.

Nkwama alifurahishwa pia na namna watumishi wa wilaya hiyo wanavyofanya kazi ya kukutana na walimu na kuwaelimisha juu ya umuhimu wa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wao kitu ambacho kimesaidia kuendelea kuimarika kwa nidhamu ya walimu wilayani hapo.

Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mecktildis Kapinga akisisitiza jambo katika kikao cha Katibu wa TSC na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kyela kilishofanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC wilayani Kyela.

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kyela, Julius Mwambogela (katikati) akiomba kupatiwa fedha za ukarabati wa ofisi wakati Katibu wa TSC alipofanya ziara katika ofisi TSC Kyela hivi karibuni.

"Ninawapongeza pia kwa namna mnavyojitahidi kutembelea shule na kufanya mikutano na walimu ya kuwaelimisha kuhusu utumishi wao. Kwa mujibu wa taarifa yenu kwa mwaka wa fedha 2021/2022 mlikuwa na mashauri ya nidhamu manne tu, hii ni hatua nzuri inayoonesha walimu wameipokea elimu mnayoitoa. Tukiendelea kuongeza bidiii katika kuwaelimisha ninaamini miaka ijayo mashauri ya nidhamu yatapungua zaidi," alisema Katibu huyo wa TSC.

Nkwama aliongeza kuwa ni lazima TSC ngazi ya Wilaya kuhakikisha kuwa kila Mkuu wa Shule anawasilisha taarifa zinazohusu masuala ya utumishi wa walimu anaowasimamia kwa kuwa wakuu hao ni mamlaka ya

TSC KYELA YAONGEZA UBUNIFU KUHUISHA TANGE YA WALIMU

kwanza ya nidhamu kwa walimu.

"Kama tutapata taarifa kutoka shuleni kwa kila robo mwaka, itarahisisha kubaini changamoto zao na kuzitatua kwa wakati," alisema.

Naye Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kyela, Julius Mwambogela alisema kuwa Wilaya hiyo ina jumla ya walimu 1670 ambapo katika idadi hiyo walimu 992 ni wa shule za msingi na 708 ni wa shule za sekondari huku akiongeza kuwa wilaya hiyo ina jumla ya shule za msingi 103 na sekondari 23 zinazosimamiwa na TSC kwa mujibu wa sheria.

Mwambogela alisema pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Ofisi hiyo inakabiliwa na uchakavu mkubwa wa jengo la ofisi jambo ambalo linawalazimu kuendelea kuwahudumia walimu katika mazingira ambayo siyo rafiki, hivyo alimuomba Katibu wa TSC kuwezesha ofisi hiyo kufanya ukarabati wa jengo.

Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (kushoto) akizungumza na Mkuu wa Idara ya Utumishi na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kuhusu umuhimu wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kufanya kazi kwa karibu na Ofisi ya TSC katika kuwahudumia walimu wilayani hapo.

Kikao cha Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (kushoto) na Mkuu wa Idara ya Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kikiwa kinaendelea. Wengine ni Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kyela, Julius Mwambogela (wa kwanza kulia) na Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mecktildis Kapinga (wa pili kutoka kulia).

Katibu wa TSC aliridhia ombi hilo na kuahidi kuwa fedha ya ukarabati wa jengo hilo itawasilishwa kwenye ofisi hiyo kabla ya Agosti 10, 2022 ili ukarabari ufanyike kwa haraka na walimu waweze kuhudumiwa katika mazingira bora.

Katika ziara hiyo, Nkwama alifanya mazungumzo na Afisa Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ambapo alimweleza kuridhishwa kwake na ushirikiano uliopo kati ya TSC na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo na kusisitiza kuwa ofisi hizo zinapaswa kuendelea kufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu ili kutoa huduma stahiki kwa walimu na kutimiza matakwa ya Kifungu cha 14 (3) cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya Mwaka 2015.

KATIBU TSC ATEMBELEA TIMU YA KUJENGA MFUMO WA TSCMIS MKOANI MOROGORO

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kulia mwenye miwani), akipewa maelezo ya hatua iliyofikiwa katika utegenezaji wa mfumo wa kielektroniki wa TSC (TSCMIS) wakati alipowatembelea wataalamu waliokuwepo mkoani Morogoro kutengeneza mfumo huo.

Na Mwandishi Wetu – Morogoro .

Katibu wa Ofisi ya Rais - Tume ya Utumishi wa Walimu (PO-TSC), Mwl. Paulina Mbena Nkwama, tarehe 13.08.2022 alitembelea timu ya maafisa na wataalamu wa TEHAMA kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali walikuwa mkoani Morogoro kwa kazi maalumu ya kutengeneza mfumo wa kielektroniki kwa dhumuni la kurahisisha na kuboresha zaidi utoaji huduma kwa Walimu wote ambao ni Watumishi wa Umma katika Shule za Msingi na Sekondari za Umma hapa nchini.

Mfumo huo utakaojulikana kama "Teachers Service Commission Management Information System - TSCMIS" tangu kuanza kuundwa kwake umegharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukiwa na moduli sita (6) zilizokamilika mpaka ulipofikia zikiwa katika hatua ya majaribio.

Pamoja na kuitembelea timu hiyo ya wataalamu akiwa ameambatana na Mkuu wa Kitengo cha Mipango, Uchumi na Ufuatiliaji, Bi. Evodia Pangani, pamoja na Afisa Utumishi Mkuu, Bw. Omar Ilyas, alipitishwa kwenye hatua zote za mfumo huo ulipofikia na namna hatua hizo zitakavyokua zikifanya kazi katika utoaji huduma kwa Walimu husika.

Aidha, akizungumza na timu hiyo baada ya kupitishwa kwenye hatua zote za mfumo huo ambazo zimekamilika, aliwashukuru kwa kazi kubwa iliyofanyika na

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kulia mwenye miwani), akipewa maelezo ya hatua iliyofikiwa katika utegenezaji wa mfumo wa kielektroniki wa TSC (TSCMIS) wakati alipowatembelea wataalamu waliokuwepo mkoani Morogoro kutengeneza mfumo huo.

KATIBU TSC ATEMBELEA TIMU YA KUJENGA MFUMO WA TSCMIS MKOANI MOROGORO

Wasilisho la hatua iliyofikiwa katika utegenezaji wa mfumo wa kielektroniki wa TSC (TSCMIS) likiendelea kutolewa wakati Katibu wa TSC, Paulina Nkwama alipofanya ziara Mkoani Morogoro ambapo ndipo kazi hiyo ilipokuwa inafanyikia.

inayoendelea kufanyika katika hatua ya kuimarisha na kuboresha mazingira ya utoaji huduma kwa Walimu hapa nchini.

Mwalimu Nkwama alisema baada ya kukamilika kwa uundaji wa mfumo ni vema lugha inayotumika katika mfumo huo ikawekwa pia kwa Kiswahili (Lugha ya Taifa) ili kurahisisha zaidi matumizi.

Vilevile, Katibu huyo alisema ni vema wataalamu wakaainisha kwa watumiaji na uongozi changamoto zinazoweza kusababisha ukwamishaji wa mfumo huo ili kuwa na mikakati ya kuzitatua kwa wakati kabla ya kuanza matumizi ya mfumo huo.

Alitoa wito kwa timu na wadau kuendelea kuangalia mwendelezo wa mfumo huo ili kukamilisha kazi hiyo.

Nae Mratibu na Msimamizi wa kazi hiyo ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa Tume hiyo, Bi. Kainda Ndassa, akitoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizoibuliwa baada ya wasilisho la mfumo huo alisema baada ya kukamilika kwa uundaji wa mfumo yatafanyika mafunzo ya awali kwa watumiaji kutoka mikoa ya kwanza minne; Dodoma, Iringa, Mwanza na Dar Es Salaam ambapo Wakuu wa Shule, Maafisa kutoka TSC Wilaya na Makao Makuu pamoja na sehemu ya wadau watashiriki mafunzo hayo kabla ya uzinduzi.

Moduli sita zilizokamilika ni pamoja na *'Disciplinary, Appeal, Gratuity and Pension Computation, Complaints, Registration, Visitors and Helpdesk.'*

Hata hivyo, timu hiyo ilikamilisha kazi hiyo na kuiwasilisha kwenye Menejimenti ya Tume tarehe 31/08/2022 ambapo wajumbe walitoa maoni na maboresho mbalimbali ili yafanyiwe kazi kabla ya kuendelea na hatua zinazofuata.

Wasilisho la hatua iliyofikiwa katika utegenezaji wa mfumo wa kielektroniki wa TSC (TSCMIS) likiendelea kutolewa wakati Katibu wa TSC, Paulina Nkwama alipofanya ziara Mkoani Mrogoro ambapo ndipo kazi hiyo ilipokuwa inafanyikia.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na wataalamu waliokuwa wanatengeneza mfumo wa kielektoniki wa TSC (TSCMIS) wakati alipowatembelea wataalamu hao mjini Morogoro hivi karibuni.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (mwenye kompyuta mpakato) akiongoza kikao cha Menejimenti ya TSC cha kupitia mfumo wa kielektroniki wa TSC (TSCMIS) kilichofanyika Agosti 31, 2022 katika ofisi za TSC Dodoma.

Wataalam wa TSC waliohusika kuandaa mfumo wa TSCMIS, Pastory Munyaki (kushoto), Laurence Chankan (katikati) na Jenipha Maagi wakitoa wasilisho la mfumo wa TSCMIS kwenye kikao cha Menejimenti kilichofanyika Agosti 31, 2022 katika ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (mwenye kompyuta mpakato) akiongoza kikao cha Menejimenti ya TSC cha kupitia mfumo wa kielektroniki wa TSC (TSCMIS) kilichofanyika Agosti 31, 2022 katika ofisi za TSC Dodoma.

Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA na Takwimu, Kainda Ndasa akitoa utangulizi kuhusu mfumo wa TSCMIS kwenye Kikao cha Menejimenti cha TSC kupitia mfumo huo kilichofanyika Agosti 31, 2022 katika ofisi za TSC Dodoma.

Wajumbe wa Kikao cha Menejimenti cha TSC wakifuatilia kwa karibu wasilisho la Mfumo wa TSCMIS kwenye kikao kilichofanyika Agosti 31, 2022.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Elimu – Kibaha, Robert Shilingi akisaini kitabu cha wageni alipotembelea banda la TSC katika Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima, Wafugaji na Wavuvi (Nanenane) yaliyofanika katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya hivi karibuni. Pembeni yake ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama.

Mtumishi wa TSC, Asha Lubuva akitoa maelezo kwa mteja aliyetembelea banda la TSC kwenye maonesho ya Nanenane yaliyofanyika jijini Mbeya mapema mwezi Agosti, 2022.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akitoa ufafanuzi kwa wateja waliofika kwenye banda la TSC kwenye maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya hivi karibuni.

Mteja akisikiliza maelezo kutoka kwa watumishi wa TSC alipotembelea banda la TSC kwenye maonesho ya Nanane yaliyofanyika jijini Mbeya hivi karibuni.

Mtumishi wa TSC, Asha Lubuva akitoa maelezo kwa mteja aliyetembelea banda la TSC kwenye maonesho ya Nanenane yaliyofanyika jijini Mbeya mapema mwezi Agosti, 2022.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Elimu – Kibaha, Robert Shilingi (kulia) na Kaimu Meneja Mkuu wa Shirika la Masoko ya Kariakoo, Sigsibert Valentine (kushoto) katika maonesho ya Nanenane yanayoendelea jijini Mbeya.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (wa nne kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya watumishi kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI na Taasisi zilizo chini ya TAMISEMI katika maonesho ya Nanenane yaliyofanyika jijini Mbeya mapema mwezi Agosti, 2022.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (wa nne kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC waliokuwepo kwenye maonesho ya Nanenane jijini Mbeya.

Watumishi wa Taasisi mbalimbali zilizopo chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) wakiwa kwenye picha ya pamoja katika maonesho ya Nanenane yaliyofanyika jijini Mbeya hivi karibuni.

TSC ILIVYOHUDUMIA WATEJA MAONESHO YA NANENANE

Wateja wakifurahi baada ya kuridhishwa na huduma inayoendelea kutolewa na watumishi wa TSC waliopo kwenye maonesho ya Nanenane jijini Mbeya.

Na. Mwandishi Wetu – Mbeya

Katika maonesho ya Nanenane jijini Mbeya yaliyofanyika Agosti 1-8, 2022, banda la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) lililokuwepo katika viwanja vya John Mwakangale liliendelea kupokea wateja kwa wingi waliofika kupata huduma mbalimbali zinazotolewa na TSC.

Miongoni mwa wateja waliotembelea banda hilo ni walimu ambao walitaka kupata ufafanuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu huduma za kiutumishi kwa walimu wa shule za msingi na sekondari za Serikali.

Miongoni mwa masuala yaliyoulizwa kwa upande wa huduma kwa walimu ni namna mchakato wa usajili wa walimu unavyofanyika, vigezo vinavyotumika kumthibitisha kazini mwalimu, taratibu za kupanda vyeo/madaraja, mchakato wa kubadilisha kazi/cheo baada ya mwalimu kujiendeleza kimasomo pamoja na hatua za kuzingatia pale mwalimu anapohitaji kustaafu kazi.

Vilevile, wateja walipata fursa ya kujua mchakato wa mashauri ya nidhamu yanavyofanyika kuanzia ngazi ya Shule, TSC Wilaya, TSC Makao Makuu pamoja na haki ya kukata Rufaa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pale ambapo mwalimu hakuridhika na uamuzi wa rufaa yake unaofanywa na TSC Makao Makuu.

Pamoja na maelezo na ufafanuzi unaotolewa, wateja wamepatiwa vipeperushi vyenye maelezo zaidi kuhusu TSC na huduma zake ili waendelee kujisomea na kupata uelewa mpana wa haki na wajibu wa mwalimu ambaye ni Mtumishi wa Umma.

Mtumishi wa TSC, Efraem Kamendu (katikati kwa waliovaa vitambulisho) akitoa ufafanuzi kwa wateja waliofika kwenye banda la TSC lililopo katika maeonesho ya Nanenane jijini Mbeya.

Mtumishi wa TSC, Donatus Nungu (wa kwanza kulia) akitoa ufafanuzi wa masuala ya Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa wateja waliotembelea banda la TSC kwenye maonesho ya Nanenane yanayofanyika jijini Mbeya.

Mtumishi wa TSC, Mecktildis Kapinga (wa kwanza kulia) akitoa ufafanuzi kwa wateja waliotembelea banda la TSC kwenye maonesho ya Nanenane yanayofanyika jijini Mbeya.

Watumishi wa TSC (waliopo upande wa kulia), Asha Lubuva na Efraem Kamendu wakimsililiza mteja aliyetembelea banda la TSC katika maonesho ya Nanenane yanayofanyika jijini Mbeya.

KATIBU TSC AIPONGEZA SHULE YA SEKONDARI TABORA WAVULANA KWA UFAULU MZURI KIDATO CHA SITA

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akiwa katika mazungumzo na Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Tabora, Mwl. Deogratias Mwambuzi yaliyofanyika hivi karibuni katika ofisi za Shule hiyo mjini Tabora.

Na Mwandishi wetu – Tabora

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama amepongeza uongozi wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Tabora maarufu kwa Jina la Tabora School liyoko Manispaa ya Tabora kwa kufanya vizuri katika matokeo ya Taifa ya Mtihani wa Kidato cha Sita.

Shule hiyo imekuwa ya pili kwa shule za Serikali na imeshika nafasi ya tatu kwa shule zote ikijumuisha za serikali na zisizo za Serikali Kitaifa kwa mwaka 2022.

Nkwama alitoa pongezi hizo hivi karibuni alipofika shuleni hapo na kufanya mazungumzo na Mkuu wa Shule hiyo, Mwl. Deogratias Mwambuzi wakati wa ufunguzi wa michezo ya shule za sekondari (UMISSETA) ambayo kitaifa inafanyikia mjini Tabora.

Shule hiyo ilikuwa na jumla ya wanafunzi 155 waliofanya mtihani wa kidato cha sita ambapo katika idadi hiyo wanafunzi 154 walifaulu kwa kiwango cha daraja la kwanza (division one) na mwanafunzi mmoja alifaulu kwa kiwango cha daraja la pili (division two).

Nkwama alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa kipaumbele kikubwa katika kuimarisha Sekta ya Elimu na ndiyo maana imeamua kupeleka fedha nyingi shuleni ili kuhakikisha miundombinu ya elimu inaboreshwa na wanafunzi wanapata taaluma kama ilivyokusudiwa.

"Ninyi mmeonesha kuwa fedha inayotolewa na Serikali yetu kwenye sekta yetu ya elimu inaweza kuleta matunda mazuri kwa kuhakikisha kila mwanafunzi anapata ujuzi na Maarifa kama ilivyokusudiwa. Kwa matokeo haya mnamtia moyo Mhe. Rais kwa kumuonesha faida ya jitihada zake," alisema Nkwama.

Katibu huyo aliongeza kuwa pamoja na mikakati mizuri ya shule hiyo, ufaulu wa wanafunzi umetokana na jitihada za walimu kufanya kazi kwa moyo

KATIBU TSC AIPONGEZA SHULE YA SEKONDARI TABORA WAVULANA KWA UFAULU MZURI KIDATO CHA SITA

wa kujitolea na uzalendo, hivyo ni muhimu kwa shule hiyo kushirikisha wadau mbalimbali na kuona namna ya kuwapa motisha walimu hao ili waendelee kuongeza juhudi zaidi katika kufundisha wanafunzi.

"Unajua unaeweza ukawa na mipango mizuri lakini kama watekelezaji wa mipango hiyo hawana moyo wa kuitekeleza huwezi kufanikiwa. Kwa ufaulu huu, ninaamini walimu wametumia hata muda wao wa ziada kufundisha, kufuwatilia na kuhakikisha kila mwanafunzi ameelewa kile alichofundishwa. Hivyo, ni vyema kutambua juhudi zao kwa namna itakayowapa morali zaidi katika kutekeleza majukumu yao," alisema.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akimsikiliza Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Tabora Mwl. Deogratias Mwambuzi katika mazungumzo yao yaliyofanyika katika shule hiyo hivi karibuni.

Vilevile, Nkwama alimshauri Mkuu huyo wa Shule kuwa na utaratibu wa kusaidia shule zingine za jirani ambazo bado hazifanyi vizuri ili nazo ziweze kutumia mbinu na mikakati ya Shule ya Wavulana Tabora na hatimaye wanafunzi wapate elimu bora.

Pia alisisitiza kuwa shule isiishie katika kuongeza taaluma peke yake bali iweke mikakati mathubuti ya kuendeleza michezo na kuwasaidia wanafunzi wenye vipaji katika michezo mbalimbali ili waweze kutumia fursa zilizopo kwa manufaa yao, shule na Taifa kwa kuwa katika dunia ya sasa michezo ni kazi inayoleta maendeleo kama zilivyo kazi nyingine.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akimpongeza Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Tabora, Mwl. Deogratias Mwambuzi kwa shule yake kufanya vizuri katika matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita kwa mwaka 2022 ambapo imeshika nafasi ya tatu Kitaifa.

"Mipango na mikakati yenu mliyojiwekea kwa upande wa taaluma imefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Lakini tukiangalia bado zipo shule zinazowazunguka ambazo hazijafanya vizuri sana kitaaluma. Sasa ni vyema mkawashirikisha wenzenu mbinu zenu ili nao wazitumie na hatimaye tuone nao wanafanya vizuri," alisema.

Aliongeza kuwa, "Pamoja na jitihada zenu katika taaluma, ni vyema muweke mipango

KATIBU TSC AIPONGEZA SHULE YA SEKONDARI TABORA WAVULANA KWA UFAULU MZURI KIDATO CHA SITA

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali wa elimu nje ya jengo la utawala la Shule ya Sekondari ya Wavulana Tabora. Viongozi hao walihudhuria ufunguzi wa michezo ya wanafunzi wa shule za sekondari (UMMISETA) uliyofanyika katika uwanja wa shule hiyo hivi karibuni.

na mikakati pia katika kuinua michezo mbalimbali kwa wanafunzi. Kama tunavyojua kwenye dunia ya sasa michezo ni ajira, michezo ni biashara, tukiwekeza vizuri katika michezo tutawasaidia wanafunzi wetu kupata fursa mbalimbali zilizopo huko nje na kuleta heshima kwenye taifa letu."

Kwa upande wake Mkuu wa Shule hiyo, Deogratias Mwambuzi alisema kuwa mafanikio ya shule hiyo yametokana na mikakati waliyojiwekea pamoja na utayari wa walimu katika kubadilisha mbinu za ufundishaji ili kukidhi matarajio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuendeleza elimu.

Alieleza kuwa mbinu ya kwanza katika mafanikio ya shule hiyo ni kila mwalimu kujiwekea malengo ya utendaji kazi na kuhakikisha anayafikia huku akieleza kuwa shule hiyo haijajiwekea lengo la kushika nafasi flani kitaifa bali lengo ni kila mwalimu kufuta alama D na F kwenye somo lake na hivyo lengo la shule ni wanafunzi wote kufalu kuanzia alama C kwa kila somo.

"Hili limetusaidia kufanya vizuri maana kila mwalimu anapimwa kwa kuangalia lengo lake ikilinganishwa na ufaulu wa wanafunzi. Walimu wetu wamelisimamia hilo kwa nguvu kubwa kwa kufanya ufuatiliaji kwa mwanafunzi mmoja mmoja kuhakikisha amepata ujuzi unaohitajika kwa kile alichofundisha na mwisho tumejikuta mwanafunzi mmoja tu ndiye kapata daraja la pili wakati wengine wote wamepata daraja la kwanza," alisema.

Alieleza kuwa mkakati mwingine walionao ni kuhakikisha mwalimu anapotunga mtihani wowote hata kama ni wa kidato cha kwanza unapitiwa na walimu wote wa idara inayohusika na somo hilo kuona kama mtihani huo unakidhi vigezo

KATIBU TSC AIPONGEZA SHULE YA SEKONDARI TABORA WAVULANA KWA UFAULU MZURI KIDATO CHA SITA

walivyojiwekea.

Sababu nyingine ya mafanikio ya shule hiyo ni mkuu wa shule hiyo kuwa karibu na walimu na kusaidia kutatua changamoto zao pale zinapojitokeza pamoja na kufuatilia utendaji kazi wa mwalimu mmoja mmoja huku yeye mwenyewe akiwa mfano kwa kujipangia vipindi vya kufundisha.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Shule, mbinu nyingine kwa shule hiyo kufanya vizuri ni kuwepo kwa ushirikiano wa karibu kati ya wazazi na uongozi wa shule, ushirikiano huo umekwenda mbali ambapo wazazi wana mfuko wao ambao unatumika kusaidia kuwezesha utekelezaji wa masuala mbalimbali ya maendeleo katika shule hiyo.

Mwl. Mwambizi alifafanua kuwa mpango anaoendelea nao sasa shuleni hapo ni kuendelea kujenga utamaduni wa walimu wake kufanya kazi wenyewe bila kusimamiwa ili hata pale anapokuwa nje ya shule walimu waendelee kujisimamia wenyewe na kuondoa dhana kuwa pengine wanajituma tu kwa kuwa wanaangaliwa na kiongozi wao.

Kuhusu suala la motisha kwa walimu, Mkuu huyo wa shule alisema baada ya matokeo hayo kutoka aliwapa walimu motisha ya ndani ambapo walikwenda sehemu na kupata chakula kwa pamoja na kubadilishana mawazo kuanzia asubuhi hadi jioni, hata hivyo alieleza kuwa kwa siku za hivi karibuni anatarajia kuwapeleka walimu hao visiwani Zanzibar kwa ajili ya kufanya utalii ikiwa ni njia ya kuwatia moyo katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kuhusu michezo alieleza kuwa amepokea ushauri wa Katibu huyo wa TSC na kuahidi kuufanyia kazi mapema iwezekanavyo ili shule hiyo ifanye vizuri kwenye taaluma na michezo pia.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (mwenye kofia nyeupe na miwani) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wanafunzi kutoka Mkoa wa Shinyanga waliohudhuria michezo ya wanafunzi wa shule za sekondari (UMMISETA) inayofanyika mjini Tabora.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule akiwa kwenye banda la Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) lililojumuisha Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Ofisi hiyo ikiwemo Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika maonesho ya Nanenane Kanda ya Kati yaliyofanyika jijini Dodoma Agosti 1- 8, 2022.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule akimkabidhi cheti cha mshindi wa kwanza katika kundi la Wizara za Sekta ya Huduma za Jamii afisa kutoka banda la OR – TAMISEMI baada ya Ofisi hiyo na Taasisi zake kuibuka mshindi katika Sherehe za Sikukuu ya Wakulima – Nanenane kwa mwaka 2022 kwa Kanda ya Kati zilizofanyika Agosti 1 – 8, 2022 jijini Dodoma.

Cheti cha mshindi wa kwanza katika kundi la Wizara za Sekta ya Huduma za Jamii kilichotolewa kwa OR – TAMISEMI na Taasisi zake baada kuibuka mshindi katika Sherehe za Sikukuu ya Wakulima – Nanenane kwa mwaka 2022 kwa Kanda ya Kati zilizofanyika Agosti 1 – 8, 2022 jijini Dodoma.

Picha ya pamoja ya watumishi walioshiriki Sherehe za Sikukuu ya Wakulima – Nanenane kwa mwaka 2022 kwa Kanda ya Kati zilizofanyika Agosti 1 – 8, 2022 jijini Dodoma.

WALIMU 99 WAPANDISHWA VYEO KIGAMBONI

Na Mwandishi Wetu – Dar es Salaam.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kigamboni iliyoko Mkoa wa Dar es Salaam imewapandisha madaraja/ vyeo walimu 99 wa shule za msingi na sokondari katika mwaka wa fedha 2021/2022 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448.

Taarifa hiyo imetolewa na Afisa Maadili na Nidhamu ya Walimu wa Wilaya ya Kigamboni, Mwl. Joyce Mwanga kwa niaba ya Kaimu Katibu Msaidizi wa wilaya hiyo wakati jarida la Sauti ya TSC lilipofanya ziara wilayani hapo hivi karibuni.

Mwl. Mwanga alieleza kuwa katika idadi hiyo ya walimu waliopandishwa madaraja 44 ni wa shule za msingi na walimu 55 ni wa shule za sekondari

Afisa wa TSC Wilaya ya Kigamboni anayeshughulikia Maadili na Nidhamu ya Walimu, Joyce Mwanga (kushoto) akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami wakati wa ziara iliyofanywa na Chami katika ofisi za TSC Kigamboni hivi karibuni.

huku akieleza kuwa malamiko ya walimu yaliyokuwepo miaka ya nyuma kutokana na kutopandishwa madaraja sasa yamekwisha.

"Katika walimu 44 wa shule za msingi tuliowapandisha, 14 ni wanaume na 30 ni wanawake na katika walimu 55 wa shule za sekondari 30 ni wanaume na 25 ni wanawake. Kwa upande wa Wilaya yetu, malalamiko ya walimu yamepungua sana, miaka ya nyuma asilimia kubwa ya malalamiko ya walimu yalikuwa yanahusu kutopandishwa madaraja licha ya kuwa na sifa, lakini kwa sasa malalamiko hayo hayapo tena," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (kulia) akiongea na Afisa wa TSC Wilaya ya Kigamboni anayeshughulikia Maadili na Nidhamu ya Walimu, Joyce Mwanga wakati wa ziara iliyofanywa na Chami katika ofisi za TSC Kigamboni hivi karibuni.

Aliendelea kufafanua kuwa kutokana na Serikali kuwajali walimu na kuwatimizia mahitaji yao kwa wakati, walimu wilayani hapo wamekuwa na morali ya kufanya kazi kwa bidii kitu ambacho kimesababisha wanafunzi kufundishwa kwa bidii huku nidhamu ya walimu ikiendelea kuimarika.

"Walimu wengi wanafanya kazi kwa kujituma hasa baada ya

WALIMU 99 WAPANDISHWA VYEO KIGAMBONI

kuona namna Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan inavyotatua changamoto zao pamoja na kuboresha miundombinu ya elimu. Ukiangalia hata kwa upande wa nidhamu, walimu wetu wanatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa taratibu, kwa kiasi kikubwa mashauri ya nidhamu yamepungua," alifafanua.

Kwa upande wa kubadilishia walimu kazi/cheo baada ya kujiendeleza kielimu, Afisa huyo alieleza kuwa ofisi hiyo tayari imepokea maombi 33 ya walimu wakiomba kubadilishiwa vyeo katika ngazi mbalimbali ambapo alieleza kuwa maombi 28 ni ya walimu wa shule za msingi na 5 ni ya wamimu wa shule za sekondari.

"Kwa zoezi la hivi karibuni kwa kuwa waliokuwa wameomba tuliwabadilishia katika zoezi lililofanyika mwezi Juni hadi Oktoba, 2021. Hata hivyo, kwa sasa tayari tumepokea maombi 33 ya walimu wanaotaka kubadilishiwa cheo na tutayafanyia kazi kwa mujibu wa taratibu ili tuwabadilishie kwa wakati", alieleza.

Afisa wa TSC Wilaya ya Kigamboni, Melkizedeck Ruambo (kushoto) akiongea jambo na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami hivi karibuni katika ofisi za TSC Kigamboni.

Ofisi hiyo inajivunia kuwa walimu wengi katika Wilaya hiyo wamekuwa na uelewa kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu kutokana na kazi kubwa ya kutoa elimu inayofanywa na watumishi wa TSC katika wilaya hiyo.

"Tumewafikia walimu wengi na kuwapa elimu juu ya sheria kanuni na taratibu za utumishi wa walimu, hata kwenye Wiki ya Utumishi wa Umma iliyofanyika mwezi Juni, 2022 tulizunguka na Afisa Utumishi na tuliwakusanya walimu kwenye Kata na tulizungumza nao kuhusu haki na wajibu wao," alisema.

Wilaya ya Kigamboni ina jumla ya shule za serikali 50 ambapo shule za msingi ni 35 na sekondari ni 15 huku shule hizo zikihudumiwa na jumla ya walimu 1125 ambapo walimu 648 ni wa shule za msingi na walimu 477 ni wa sekondari.

Watumishi wa TSC Wilaya ya Kigamboni, Melkizedeck Ruambo (kushoto) na Joyce Mwanga (katikati) wakimsikiliza Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami wakati wa ziara ya Chami katika ofisi ya TSC Kigamboni hivi karibuni.

UBORA WA HUDUMA ZA TSC WAWA KIVUTIO KWA WATEJA MAONESHO YA NANENANE

Mtumishi wa TSC, Mecktildis Kapinga (aliyening'iniza kitambulisho) akitoa maelezo kwa wateja waliotembelea maonesho ya Nanenane jijini Mbeya. Pembeni yake ni Afisa Sheria wa TSC, Donatus Nungu.

Na Mwandishi wetu – Mbeya.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliendelea kupokea idadi kubwa ya wateja wanaotembelea banda lake lililokuwa ndani Uwanja wa John Mwakangale katika maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Kitaifa jijini Mbeya.

Idadi ya watu waliotembelea banda hilo imeendelea kuongezeka kutokana na ubora wa huduma zilizokuwa zinazotolewa na watumishi wa TSC kwenye banda la Tume hiyo inayosimamia Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari walio kwenye Utumishi wa Umma ambao idadi yao ni zaidi ya nusu ya watumishi wa Umma nchini.

Watumishi wanaotoa huduma kwenye banda hilo ni Mecktildis Kapinga ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu, Efraem Kamendu, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mbeya, Donatus Nungu, Afisa Sheria pamoja na Asha Lubuva ambaye ni Afisa anayeshughulikia Maadili na Nidhamu ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu.

Baadhi ya wateja waliofika kwenye banda la TSC walieleza kuwa walitembelea banda hilo baada ya kupata taarifa kutoka kwa wenzao ambao ni walimu walioridhishwa na elimu waliyoipata pamoja na kutatuliwa changamoto za kiutumishi zilizokuwa zinawakabili.

"Kuna wenzetu walikuja jana walikuwa na changamoto za kiutumishi, walitueleza kuwa walipokelewa vizuri, wakasikilizwa na kupatiwa ufumbuzi wa changamoto zao. Lakini pia walituambia walipatiwa elimu ya mambo mbalimbali yanayohusu utumishi wa mwalimu ambayo hawakuwa na uelewa nayo. Hivyo, na sisi tukaona tufike wenyewe kwa kuwa tunahitaji huduma pamoja na kupata uelewa mpana juu ya utumishi wetu," alisema mmoja wa wateja ambaye ni mwalimu.

Baada ya kupatiwa huduma, wateja hao walionesha kuridhishwa na namna changamoto zao zilivyofanyiwa kazi pamoja na kupatiwa elimu zaidi ya masuala ya kiutumishi

Wateja wakiendelea kuhudumiwa wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika jijini Mbeya hivi karibuni.

UBORA WA HUDUMA ZA TSC WAWA KIVUTIO KWA WATEJA MAONESHO YA NANENANE

huku wakiahidi kuwa mabalozi wazuri wa kuwahabarisha wenzao ili wafike kwenye banda hilo kupata huduma za TSC.

"Tumehudumiwa vizuri na pia tumepatiwa elimu ya mambo mengi ambayo hatukuwa na uelewa nayo. Elimu tuliyoipata hapa itatusaidia kutekeleza majukumu yetu ya ualimu, hivyo tutazingatia sheria, kanuni na taratibu katika kufundisha wanafunzi," alieleza mmoja wa wateja waliotembelea banda hilo.

Mbali na kutembelewa na walimu, banda la TSC limeendelea kuwa kivutio kwa wateja wa aina mbalimbali ambao wanafika kwa lengo la kupata uelewa juu ya kazi zinazofanywa na Tume hiyo kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2016.

Wateja wakiendelea kuhudumiwa wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika jijini Mbeya hivi karibuni.

Mwonekano wa banda ambalo TSC ilikuwemo wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika jijini Mbeya.

KATIBU TSC ATOA WIKI MOJA KWA TSC WILAYA YA RUNGWE KUWASILISHA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YAKE

Na Mwandishi wetu – Rungwe.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama ametembelea ofisi ya TSC Wilaya ya Rungwe iliyopo Mkoa wa Mbeya na kutoa muda wa wiki moja kwa watumishi wa ofisi hiyo kuwasilisha kwake taarifa ya utekeezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Nkwama ametoa agizo hilo hivi karibuni wilayani hapo alipofanya ziara kwa lengo la kufanya ufuatiliaji wa namna wilaya hiyo inavyowahudumia walimu wa shule za Msingi na Sekondari za Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016.

Akiwa ofisini hapo, Nkwama alionesha kutoridhishwa na taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo iliyotolewa na mtumishi wa TSC Wilaya ya Rungwe, Paul Kazinde kutokana na kuwepo kwa mkanganyiko wa takwimu huku alieleza kuwa taarifa hiyo haikuzingatia mwongozo wa uwasilishaji wa taarifa uliotolewa na TSC Makao Makuu.

"Kwa kweli sijaridhishwa na namna taarifa yenu mlivyoiandaa, tulileta kwenu mwongozo wa namna ya kuandaa taarifa lakini hapa hamjazingatia. Hata takwimu mnazotoa hazipo sawa, zingatieni utaratibu uliotolewa kwani ni njia rahisi ya kuandaa taarifa inayokidhi mahitaji. Hivyo, ninawapa wiki moja muwasilishe kwangu taarifa iliyokamilika na iliyozingatia mwongozo unaotumika," alisema Nkwama.



Kiongozi huyo aliendelea kueleza kuwa Ofisi za Wilaya zinatakiwa kuwa kimbilio la walimu na hivyo ni wajibu wa watumishi wa TSC ngazi ya Wilaya kuhakikisha wanachukua jukumu la kufuatilia masuala ya walimu kwenye mamlaka nyingine na hatimaye kutoa mrejesho kwa mwalimu husika ili kuondoa kero na usumbufu kwa mwalimu.

"Tunataka mwalimu anapowasilisha hoja yake sisi ndio tunajukumu la kwenda kugonga milango ya ofisi zingine kufuatilia hoja yake. Hatupaswi kuanza kumwambia mwalimu fuatilia mwenyewe. Siyo sawa kuona mwalimu anaacha jukumu lake la kufundisha wanafunzi anahangaika kwenye ofisi mbalimbali kufuatilia masuala

KATIBU TSC ATOA WIKI MOJA KWA TSC WILAYA YA RUNGWE KUWASILISHA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YAKE

yake mwenyewe wakati TSC tupo. Tunapaswa tubadilike na tuache tabia ya kufanya kazi kwa mazoea," alisema Katibu huyo.

Pamoja na hayo, Katibu huyo alionesha na kuridhishwa na namna Wilaya hiyo ilivyofanya kazi ya kutoa elimu kwa walimu kitu ambacho kimesababisha hali ya nidhamu kuimarika na kupungua kwa mashauri ya nidhamu huku akieleza kuwa jitihada zaidi zinahitajika ili walimu wawajibike zaidi katika kutoa huduma kwa wanafunzi.

"Ninawapongeza kwa namna mnavyotoa elimu kwa walimu, nimefurahi kusikia mmewafikia walimu wengi na kuwapa elimu juu ya masuala yanayohusu utumishi wao. Tunapaswa kuwahamasisha zaidi walimu ili waweze kuwajibika kikamilifu katika kufundisha wanafunzi. Wakati mwingine unaweza ukajisifu kuwa walimu wamepata elimu na wananidhamu nzuri lakini kama wanafunzi hawafaulu kazi yetu inakuwa haijakamika," alisema Nkwama.

Kiongozi huyo pia alitembeleea Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ambapo alifanya mazungumzo na Mwanasheria wa Halmashauri hiyo ambaye alikuwa anamwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo.

Katika mazungumzo yao, Katibu wa TSC alieleza umuhimu wa Ofisi ya Mkurugenzi ambaye ndiye mwajiri wa mwalimu kufanya kazi kwa karibu na Ofisi ya TSC Wilaya kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 14 (3) cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya Mwaka 2015.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Dkt. Francis Michael (wa nne kutoka kushoto) akiwa na viongozi wengine wa elimu wakati akifungua mashindano ya michezo katika shule za Sekondari (UMISSETA) Agosti 11, 2022 mjini Tabora. Wa pili kutoka kushoto ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.

Picha ya pamoja kati ya viongozi wa elimu na wanafunzi wachezaji mara baada ya ufunguzi wa mashindano ya michezo katika shule za Sekondari (UMISSETA) yaliyofanyika hivi karibuni mjini Tabora.

Picha ya pamoja ya viongozi mbalimbali wa elimu wakati wa ufunguzi wa mashindano ya michezo katika shule za Sekondari (UMISSETA) yaliyofanyika hivi karibuni mjini Tabora.

Picha ya pamoja kati ya viongozi wa elimu na waamuzi wa michezo mbalimbali wakati wa mashindano ya michezo katika shule za Sekondari (UMISSETA) yaliyofanyika hivi karibuni mjini Tabora.

Picha ya pamoja ya viongozi mbalimbali wa elimu wakati wa ufunguzi wa mashindano ya michezo katika shule za Sekondari (UMISSETA) yaliyofanyika hivi karibuni mjini Tabora.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Dkt. Francis Michael (kushoto) akisalimiana na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama wakati wa ufunguzi wa mashindano ya michezo katika shule za Sekondari (UMISSETA) yaliyofanyika hivi karibuni mjini Tabora.

Naibu Katibu Mkuu (elimu) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dkt. Charles Msonde (kulia) akifurahia jambo na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) pamoja na Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora, Dkt. John Mboya (katikati) wakati wa wa ufunguzi wa mashindano ya michezo katika shule za Sekondari (UMISSETA) yaliyofanyika hivi karibuni mjini Tabora.

Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akisalimiana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora, Dkt. John Mboya wakati wa wa ufunguzi wa mashindano ya michezo katika shule za Sekondari (UMISSETA) yaliyofanyika hivi karibuni mjini Tabora.

Wanafunzi wa shule za Sekondari wakiwa kwenye burudani wakati wa ufunguzi wa mashindano ya michezo katika shule za Sekondari (UMISSETA) yaliyofanyika hivi karibuni mjini Tabora.

Wanafunzi wa shule za Sekondari wakiwa kwenye burudani wakati wa ufunguzi wa mashindano ya michezo katika shule za Sekondari (UMISSETA) yaliyofanyika hivi karibuni mjini Tabora.

TSC KINONDONI YAJIVUNIA UFAULU MZURI SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI

Na Mwandishi Wetu–Kinondoni.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kinondoni inajivunia kutokana na walimu wa Wilaya hiyo kufanya kazi kwa bidii, weledi na uzalendo kitu ambacho kimefanya Wilaya kufanya vizuri katika taaluma kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Imeelezwa kuwa katika matokeo ya mitihani ya taifa kwa mwaka 2021 ufaulu wa wanafunzi wa shule za msingi ulikuwa zaidi ya asilimia 98 huku ufaulu wa shule za sekondari kwa kidato cha nne ulikuwa ni zaidi ya asilimia 91 na ufaulu wa sekondari kwa kidato cha sita ulikuwa ni zaidi ya asilimia 97.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kinondoni, Theobald Kilindo wakati akifafanua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami wakati ziara iliyofanywa na Mkuu huyo wa Kitengo katika Wilaya ya Kinondoni hivi karibuni.

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kinondoni, Theobald Kilindo (kushoto) akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami (kulia) hivi karibuni katika ofisi za TSC Kinondoni.

Kilindo alieleza kuwa ufaulu wa wanafunzi ni kutokana na walimu wa Wilaya hiyo kufanya kazi katika mazingira mazuri kutokana na kuhudumiwa vizuri na TSC katika nyanja mabalimbali za kiutumishi ikiwa ni moja ya mikakati ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan katika kuboresha maslahi na mazingira ya kazi kwa walimu.

"Kwa mwaka 2021 kwa upande wa shule za Msingi tumeshika nafasi ya kwanza Kimkoa na nafasi ya pili Kitaifa na kwa upande wa shule za sekondari tumeshika

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami (kulia) akisisitiza jambo wakati wa kikao chake na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kinondoni, Theobald Kilindo (kushoto) kilichofanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC Kinondoni.

Watumishi wa TSC Wilaya ya Kinondoni wakimsikiliza kwa makini Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami (wa kwanza kushoto) wakati wa kikao kilichofanyika katika ofisi za TSC Kinondoni hivi karibuni.

TSC KINONDONI YAJIVUNIA UFAULU MZURI SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI

Watumishi wa TSC Wilaya ya Kinondoni wakimsikiliza kwa makini Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami (wa kwanza kushoto) wakati wa kikao kilichofanyika katika ofisi za TSC Kinondoni hivi karibuni.

nafasi ya kwanza Kimkoa. Ufaulu huu wa wanafunzi ni matunda ya jitihada za Rais wetu Mhe. Samia Suluhu Hassan katika kutatua changamoto za watumishi wakiwemo walimu ambapo na sisi TSC tumekuwa mstari wa mbele katika kutoa huduma bora kwa walimu wetu," alisema.

Alieleza kuwa TSC imekuwa ikiendelea kusimamia utumishi wa walimu ikiwemo ajira, upandishaji vyeo, kubadilishia vyeo walimu wanaojiendeleza kielimu, kusimamia maadili na nidhamu kwa walimu, kushughulikia malalamiko mbalimbali ya walimu pamoja na masuala yote yanayotekelezwa na TSC kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 na Kanuni zake za mwaka 2016.

Akizungumzia kuhusu ajira Kilindo alisema kwa mwezi Julai, 2022 jumla ya walimu 31 waliapangiwa vituo vya kazi katika Wilaya hiyo ambapo katika idadi hiyo walimu wawili (2) ni wa shule za msingi na walimu 29 ni wa shule za sekondari.

Kwa upande wa maendeleo ya walimu, Kilindo alisema kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya walimu 569 walipandishwa vyeo ambapo walimu 351 ni wa shule za msingi na waimu 218 ni wa shule za sekondari huku walimu 88 wa shule za msingi na watatu (3) wa shule za sekondari wakibadilishiwa vyeo baada ya kijiendeleza kielimu.

Kwa upande wa nidhamu Kaimu Katibu Msaidizi huyo alieleza kuwa walimu wilayani hapo wanaendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za kiutumishi kitu ambacho kimefanya Wilaya hiyo kuwa na idadi ndogo ya mashauri ya nidhamu ya walimu.

"Tukiachana na mashauri yanayohusu kughushi ambayo yalitokana na zoezi kuondoa watumishi wa umma ambao hawakuwa na vyeti halali lililofanyika nchi nzima, mashauri mengine kwa mwaka 2019/2020 yalikuwa 12, mwaka 2020/2021 yalikuwa 16, mwaka 2021/2022 yalikuwa 5. Kwa kweli tunaona kuwa walimu wanaendelea kuimarika kinidhamu," alisema.

Pamoja na nidhamu kuwa nzuri, Kilindo alisema kuwa wapo waalimu wachache ambao bado wanakwenda kinyume na maadili ya kazi ya ualimu huku akieleza kuwa kosa la utoro kazini linaongoza ambapo alieleza sababu za utoro huo kuwa ni walimu kukopa kupita kiasi na kushindwa kurejesha mikopo kitu ambacho kinawafanya waondoke kwenye vituo vya kazi kwa kuogopa kufwata na kuchukuliwa hatua na wanaowadai.

Alieleza kuwa ofisi yake inaendelea kutoa elimu kwa walimu ili kujiepusha na makosa ya kinidhamu huku akieleza kuwa wale wanaoshindwa kufuata taratibu za kiutumishi wataendelea kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ili kuhakikisha Wilaya hiyo inaendelea kufanya vizuri katika elimu.

WATUMISHI TSC WAAGIZWA KUTOA ELIMU KWA WALIMU JUU YA KUBADILISHIWA KAZI/CHEO

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akizungumza na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Uyui, Henry Wamara wakati Katibu huyo wa TSC alipofanya ziara wilayani Uyui hivi karibuni.

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Uyui, Henry Wamara akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa wajukumu ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (hayupo pichani) wakati Katibu wa TSC alipofanya ziara wilayani hapo hivi karibuni.

Na Mwandishi wetu – Tabora.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama amewaagiza watumishi wa TSC kwenye ngazi ya wilaya kuweka mkazo katika kutoa elimu kwa walimu juu ya taratibu na umuhimu wa kubadilisha cheo/kazi baada ya kujiendeleza kielimu.

Nkwama ametoa kauli hiyo wakati wa ziara yake katika ofisi ya TSC Wilaya ya Uyui mkoani Tabora aliyoifanya hivi karibuni kwa lengo la kuona namna ofisi hiyo inavyotoa huduma kwa walimu wa shule za msingi na sekondari za Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 na Kanuni zake za mwaka 2016.

Katibu alitoa agizo hilo baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kutoka kwa Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC wa Wilaya ya Uyui, Henry Wamara ambapo alielezwa kuwa hakuna mwalimu aliyebadilishiwa kazi/cheo licha ya kuwa wapo waliopewa ruhusa na mwajiri wakaenda kusoma na kuhitimu masomo yao.

Katibu wa TSC, Paulina Nkwama akimuonesha Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Uyui, Henry Wamara moja kati ya vibabu vitatu vilivyozinguliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi karibuni ikiwa ni mwendelezo wa kufanya maboresho kwenye Sekta ya Elimu nchini.

Katibu wa TSC, Paulina Nkwama akimsomea Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Uyui, Henry Wamara mwongozo mpya unaohusu masuala ya uteuzi wa wakuu wa shule za msingi na sekokari ambapo TSC ni mjumbe wa kamati ya kupendekeza majina kwa ajili ya uteuzi.

WATUMISHI TSC WAAGIZWA KUTOA ELIMU KWA WALIMU JUU YA KUBADILISHIWA KAZI/CHEO

Katibu wa TSC, Paulina Nkwama akiongea na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, Hemed Magaro (hayupo pichani) wakati wa ziara yake aliyoifanya wilayani Uyui hivi karibuni.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, Hemed Magaro akiongea na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (hayupo pichani) wakati Katibu wa TSC alipofanya ziara wilayani Uyui hivi karibuni.

Wamara alisema kuwa sababu ya walimu kumaliza masomo na kuficha vyeti badala ya kuviwasilisha kwa mwajiri ni kutokana na dhana iliyojengeka kuwa mwalimu anapobadilishiwa cheo anachelewa kupanda daraja bila kuzingatia faida za mbeleni na fursa mbalimbali anazoweza kupata ikiwa atawekwa katika muundo wake kwa usahihi kulingana na kiwango cha elimu alichonacho.

Nkwana alisema kuwa lengo la mwajiri kumruhusu mwalimu kwenda masomoni ni kumsaidia kuongeza ujuzi na maarifa katika eneo lake analofanyia kazi na inatarajiwa kuwa mwalimu huyo anapohitimu masomo yake atabadilishiwa muundo na kuweka katika cheo anaostahili kwa mujibu wa taratibu za utumishi.

Alifafanua kuwa ni wajibu wa mwalimu kuwasilisha vyeti vyake mara baada ya kuhitimu masomo yake ili Serikali iweze kufanya maboresho katika Ikama yake kwa kadiri inavyohitajika.

"Tunapaswa kuongeza juhudi za kuwaelimisha walimu kujua umuhimu na fursa wanazoweza kuzipata kwa kubadilishiwa muundo. Kuna faida nyingi kwa mwalimu kubadilishiwa kazi/cheo, lakini wengi wao bado hawajapata elimu hiyo ndiyo maana mtu amehitimu masomo yake lakini hataki kuwasilisha vyeti kwa mwajiri anaona kana kwamba akibadilishiwa muundo maendeleo ya utumishi wake yanasimama, jambo ambalo sio la kweli kabisa," alisema Nkwama.

Aliongeza kuwa, "Tunapaswa kuwa karibu na mwajiri ili pale mwalimu anaporuhusiwa kwenda masomoni sisi tuanaanza maandalizi ya kumuweka kwenye taratibu za kumbadilishia cheo na pale anaporudi tu tunamkumbusha mwajiri amwandikie barua ili awasilishe vyeti vyake na sisi TSC mara moja tunambadilishie cheo bila kuchelewa kwani ndio utaratibu."

Katibu huyo alifafanua kuwa Serikali imeamua kufanya mapinduzi makubwa kwenye sekta ya elimu kwa kuhakikisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondani wanapata ujuzi na mwalimu anapaswa kupimwa kwa namna wanafunzi wanavyoelewa kile wanachofundishwa, hivyo walimu wanajiendeleleza kielemu ili kuongeza ufanisi wa kazi yao katika kuwasaidia wanafunzi kuelewa vizuri kile wanachofundishwa.

"Moja ya njia za kufanya wanafunzi wetu wapate ujuzi kama ilivyokudiwa ni kuhakikisha kila mwalimu anapata kile anachostahili kwa mujibu wa sheria. Hivyo, ni wajibu wetu kuwaelimisha wajue umuhimu wa kuwekwa katika vyeo vyao sahihi kwa mujibu wa muundo wa utumishi wao. Tusipowasaidia walimu na kuwahudumia vizuri hawataweza kutoa huduma tunayotamani waitoe kwa wanafunzi," alisema Nkwama.

Awali, akiwasilisha taarifa ya ofisi yake, Wamara alieleza kuwa Wilaya ya Uyui ina jumla ya shule 177 ambapo katika idadi hiyo shue 150 ni za msingi na 27 ni

WATUMISHI TSC WAAGIZWA KUTOA ELIMU KWA WALIMU JUU YA KUBADILISHIWA KAZI/CHEO

za sekondari huku akieleza kuwa wilaya hiyo ina walimu 1432 wa shule za msingi na walimu 403 wa shule za sekondari na hivyo kufanya jumla ya walimu wilayani hapo kuwa1835.

"Ofisi imesimamia na kukagua ujazaji wa mikataba ya ajira kwa walimu 169 ambapo walimu 68 walisajiliwa na hatimaye kuthibitishwa kazini na walimu 101 ambao wameajiriwa mwezi Juni, 2022 taratibu za kuwasajili zinaendelea," alisema Wamara.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo aliendelea kueleza kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wilaya hiyo imewapandisha madaraja walimu 226 ambapo walimu 193 ni wa shule za msingi na walimu 33 ni wa shule za sekondari.

Kwa upande wa mashauri ya nidhamu, kiongozi huyo alieleza kuwa jumla ya mashauri 15 yalipokelewa ambapo mashauri 12 yalihusu utoro na mashauri 3 yalihusu uhusiano wa kimapenzi huku akieleza kuwa katika mashauri yaliyopokelewa, 12 yamehitimishwa na mashauri 3 yapo katika hatua za mwisho za kuhitimishwa.

Wamara alieleza changamoto zinazoikabili ofisi hiyo kuwa ni upungufu wa watumishi ambapo kwa sasa ofisi ina watumishi wawili tu na hivyo alimuomba Katibu wa TSC kuona namna ya kuongeza watumishi ili ofisi hiyo iweze kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa walimu.

"Pamoja na upungufu wa watumishi kuwa changamoto kubwa, kutokuwepo kwa chombo cha usafiri ni kikwazo kikubwa katika utekelezaji wa majukumu yetu kwa ufanisi. Ukiangalia Wilaya hii ni kubwa ikilinganishwa na wilaya zingine za Mkoa huu, hivyo kuna changamoto kubwa katika kuzifikia shule. Ninaomba pia Katibu uone namna ya kutusaidia ili tuweze kupata usafiri wa kutuwezesha kuzifikia shule zetu kwa wakati," Alisema Wamara.

Akijibu maombi hayo, Katibu wa TSC aliahidi kufanyia kazi suala la upungufu wa watumishi ili ofisi hiyo iweze kutoa huduma kwa ubora unaotakiwa huku kwenye suala la usafiri akieleza kuwa ofisi za TSC zinapaswa kuendelea kushirikiana na ofisi ya Mkurugenzi na kutumia vyombo vya usafiri kama ilivyoelekezwa na Waziri pamoja na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Pamoja na ziara yake kwenye ofisi hiyo, Nkwama alikutana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, Hemed Magaro ambapo walijadili masuala mbalimbali ya kuongeza ushirikiano katika kuwahudumia walimu ili wanafunzi wa wilaya hiyo waweze kufanya vizuri zaidi katika mitihani yao.

Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, Hemed Magaro (kulia) pamoja na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Uyui, Henry Wamara (kushoto) wakati wa ziara ya Katibu wa TSC aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.

Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (kulia) na Katibu Tawala wa Wilaya ya Uyui, Moses Tesha (katikati) wakimsikiliza Kaimu Katibu Msaidizi wa TSCWilaya ya Uyui, Henry Wamara wakati wa ziara ya Katibu wa TSC aliyoifanya wilayani Uyui hivi karibuni.

Picha ya pamoja ya Watumishi wa OR – TAMISEMI na Taasisi zake waliohudhuria maonesho ya Nanenane jijini Mbeya.

Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mecktildis Kapinga akipitia nyaraka zilizowasilishwa na mteja wakati wa maonesho ya Nanenane yaliyofanyika jijini Mbeya hivi karibuni.

Mteja aliyetembelea banda la TSC akitoa maelezo yake kwenye maonesho ya Nanenane yaliyofanyika jijini Mbeya.

Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mecktildis Kapinga (mwenye kitambulisho) akiendela kutoa huduma kwa wateleja waliotembelea banda la TSC wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika jijini Mbeya.

Watumishi wa TSC (wenye vitambulisho) wakimsikiliza mteja.

Wateja wakiendelea kuhudumiwa wakati wa maonesho ya Nanenane yaliyofanyika jijini Mbeya hivi karibuni.

TSC YAPONGEZWA KWA KUENDELEA KUTOA HUDUMA BORA KWA WALIMU

Na. Mwandishi Wetu – Mbeya

Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo Mhe. Dkt Julius Ningu ameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kuendelea kusimamia ajira, maadili, maendeleo na maslahi mbalimbali ya walimu kitu ambacho kimesaidia kuleta utulivu kwa walimu nchini.

Mkuu huyo wa Wilaya alitoa pongezi hizo Agosti 5, 2022 alipotembelea banda la TSC katika maonesho ya Nanenane yaliyofanyika jijini Mbeya huku akieleza kuwa TSC ina wajibu wa kuhakikisha kero ndogondogo zinazowakabili walimu zinafanyiwa kazi ili waendelee kuwa na moyo wa kutumikia Taifa lao.

Aliongeza kuwa Sekta ya Elimu imeendelea kuimarika kutokana na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali ikiwa ni pamoja na usimamizi mzuri unaofanywa na TSC katika kuwaelimisha walimu juu ya sheria, kanuni na taratibu za Utumishi wa Walimu na matokeo ya jitihada hizo ni pamoja na kuendelea kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari nchini.

Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo Mhe. Dkt Julius Ningu (mwenye kofia nyeupe) akisikiliza maelezo kutoka watumishi wa TSC alipotembelea banda la Tume hiyo kwenye maonesho ya Nanenane yanayofanyika Kitaifa jijini Mbeya.

Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mecktildis Kapinga (wa kwanza kushoto) akitoa maelezo kwa Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo Mhe. Dkt Julius Ningu (aliyevaa kofia nyeupe) juu ya majukumu yanayotekelezwa na TSC. Alitoa maelezo hayo wakati kiongozi huyo alipotembelea banda la TSC katika maonesho ya Nanenane yanayofanyika jijini Mbeya.

Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo Mhe. Dkt Julius Ningu (mwenye kofia nyeupe) akiwa kwenye banda la TSC.

KATIBU NA WATUMISHI TSC WAUNGANA NA KATIBU MKUU KIONGOZI BONANZA LA UHAMASISHAJI SENSA YA WATU NA MAKAZI

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Karibu kutoka Ofisi ya Rais - Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Mbena Nkwama, ndc akiwaongoza watumishi wa Tume hiyo wameungana na Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Hussein Kattanga akiwa Mgeni Rasmi katika Bonanza la Michezo ya Uhamasishaji Wananchi kujitokeza na kushiriki katika Sensa ya Watu na Makazi Agosti 23, 2022.

Bonanza hilo liliandaliwa na kuratibiwa na Shirikisho la Michezo ya Wizara na Taasisi za Umma (SHIMIWI) na kufanyika Agosti 20, 2022 lilianzia katika Viwanja vya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumalizìkia katika Viwanja vya Jamhuri ambapo Watumishi kutoka Wizara, Taasisi, Mashirika na Mamlaka mbalimbali za Serikali walishiriki mazoezi pamoja na kucheza michezo mbalimbali.

Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Hussein Kattanga akuzungumza katika Bonanza la Michezo ya Uhamasishaji Wananchi Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 lililowahusisha Watumishi kutoka Wizara, Taasisi, Mashirika na Mamlaka mbalimbali za Serikali lililofanyika katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 20, 2022.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akijitabulisha katika Bonanza la Michezo ya Uhamasishaji Wananchi Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 lililowahusisha Watumishi kutoka Wizara, Taasisi, Mashirika na Mamlaka mbalimbali za Serikali lililofanyika katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 20, 2022.

Viongozi mbalimbali wakiwa katika hali ya furaha katika Bonanza la Michezo ya Uhamasishaji Wananchi Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 lililowahusisha Watumishi kutoka Wizara, Taasisi, Mashirika na Mamlaka mbalimbali za Serikali lililofanyika katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 20, 2022.

Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Hussein Kattanga (katikati mwenye kofia, miwani na viatu vyeupe) akishiriki kufanya mazoezi ya viungo katika Bonanza la Michezo ya Uhamasishaji Wananchi Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 lililowahusisha Watumishi kutoka Wizara, Taasisi, Mashirika na Mamlaka mbalimbali za Serikali lililofanyika katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 20, 2022.

Watumishi mbalimbali wakifanya mazoezi ya viungo katika Bonanza la Michezo ya Uhamasishaji Wananchi Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 lililowahusisha Watumishi kutoka Wizara, Taasisi, Mashirika na Mamlaka mbalimbali za Serikali lililofanyika katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 20, 2022.

Watumishi mbalimbali wakifanya mazoezi ya viungo katika Bonanza la Michezo ya Uhamasishaji Wananchi Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 lililowahusisha Watumishi kutoka Wizara, Taasisi, Mashirika na Mamlaka mbalimbali za Serikali lililofanyika katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 20, 2022.

Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Hussein Kattanga (katikati mwenye kofia, miwani na viatu vyeupe) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali pamoja na waamuzi wa mchezo wa pete katika Bonanza la Michezo ya Uhamasishaji Wananchi Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 lililowahusisha Watumishi kutoka Wizara, Taasisi, Mashirika na Mamlaka mbalimbali za Serikali lililofanyika katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 20, 2022.

Mchezo wa kuvuta kamba ukiwa unaendelewa wakati wa Bonanza la Michezo ya Uhamasishaji Wananchi Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 lililowahusisha Watumishi kutoka Wizara, Taasisi, Mashirika na Mamlaka mbalimbali za Serikali lililofanyika katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 20, 2022.

Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Hussein Kattanga (wa tano kutoka kulia kwa waliosimama) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wanamichezo waliohudhuria katika Bonanza la Michezo ya Uhamasishaji Wananchi Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 lililowahusisha Watumishi kutoka Wizara, Taasisi, Mashirika na Mamlaka mbalimbali za Serikali lililofanyika katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 20, 2022.

Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Hussein Kattanga akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wanamichezo waliohudhuria katika Bonanza la Michezo ya Uhamasishaji Wananchi Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 lililowahusisha Watumishi kutoka Wizara, Taasisi, Mashirika na Mamlaka mbalimbali za Serikali lililofanyika katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 20, 2022.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (mwenye sweta lenye rangi ya kijani) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC wakioshiriki Bonanza la Michezo ya Uhamasishaji Wananchi Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 lililowahusisha Watumishi kutoka Wizara, Taasisi, Mashirika na Mamlaka mbalimbali za Serikali lililofanyika katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 20, 2022. Kushoto kwa Katibu huyo ni Kamishna wa TSC, Mwl. Susana Nussu.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania